

## **Chanjo za Kuzuia COVID-19**

Unavyoju Virusi vya korona, vinavyojulikana pia kama COVID-19, ni ugonjwa hatari uliosambaa katika kila nchi duniani. Hapa katika Rhode Island, zaidi ya watu 85,000 wameugua COVID-19, na karibu watu 1,800 wamekufa kutokana na COVID-19.

Chanjo zimeundwa ili kulinda watu dhidi ya kupata COVID-19, na wanaanza kusambaza chanjo hizo.

Chanjo ni bidhaa ambayo husaidia mwili wa mtu kuzalisha kinga ya mwili dhidi ya ugonjwa, yaani, mara tu mtu amepokea chanjo, anaweza kuwa wazi kwa ugonjwa huo bila kuambukizwa.

Chanjo ni muhimu kwa sababu hailindi tu mtu anayepata chanjo hiyo, lakini pia inasaidia kuzuia magonjwa dhidi ya kusambaa kwa watu wengine, kama wanafamilia, majirani, wanafunzi wenza, na wanachama wengine wa jumuiya yako.

Chanjo mpya za COVID-19 zimepimwa kabisa kwa usalama kabla ya kuidhinishwa kwa matumizi Marekani. Chanjo za COVID-19 hazina virusi vilivyo hai na hazina hatari ya kusababisha ugonjwa kwa mtu aliyepewa chanjo.

Chanjo za COVID-19 zinazotumika Marekani zinahitaji dozi mbili. Dozi ya kwanza huanza kuunda ulinzi, lakini kila mtu lazima arudi baada ya wiki chache baadaye kwa ajili ya dozi ya pili ili kupata ulinzi zaidi ambao chanjo hiyo hutoa.

Watu wengi hawana matatizo makubwa baada ya kupewa chanjo. Baadhi ya madhara ambayo watu wamekuwa nayo ni kuwa mkono wako unaweza kuvimba, kuwa mwekundu, au wenye joto ukiguswa. Dalili hizi mara nydingi hupotea peke yao ndani ya wiki. Baadhi ya watu huripoti kuumwa na kichwa au kuwa na homa wanapopata chanjo. Madhara haya ni dalili kuwa mfumo wa kingamwili wa mwili wako unafanya kazi inayopaswa kufanya. Inafanya kazi na kuunda ulinzi kwa ugonjwa.

Dozi za chanjo zilizonunuliwa na pesa za mlipa ushuru wa Marekani zitapeanwa kwa kila mtu bila gharama yoyote. Hata hivyo, watoaji wa chanjo wataweza kutoza ada ya kuchanja mtu chanjo hiyo. Watoaji wa chanjo wanaweza kurudishiwa ada hii na kampuni ya bima ya umma au ya kibinagsi ya mgongwa huyo au, kwa wagonjwa ambao hawana bima, na Rasilimali na Huduma za Afya Fedha za Msaada za Mtoaji Chanjo.

Kila jimbo lina mpango wake wenyewe wa atakayepata chanjo kwanza na jinsi chanjo zitakavyosambazwa. Wahudumu wa afya na watu wazee watapewa chanjo kwanza. Zaidi ya usambazaji huu wa kwanza Jimbo la Rhode Island litatoa mielekeo zaidi katika siku zijazo. Pata maelezo zaidi katika [www.C19vaccineRI.org](http://www.C19vaccineRI.org)